

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



**TAKUKURU MKOA WA KAGERA YAMPANDISHA KIZIMBANI
MTUMISHI WA TANESCO**

TAARIFA KWA UMMA

NOVEMBER 5, 2020

Ndugu wanahabari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera tumeendelea kutekeleza majukumu yetu kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sheria namba 11 ya mwaka 2007. Katika utekelezaji wa majukumu yetu tumeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa mapambano dhidi ya Rushwa wakiwemo waandishi wa habari, viongozi wa Serkali na wananchi kwa ujumla. Aidha majukumu haya yametokelezwa katika wilaya zote zilizoko ndani ya Mkoa wa Kagera.

Ndugu wanahabari,

Tunapenda kuujulisha umma kuwa leo tarehe 05/11/2020 **TAKUKURU** mkoa wa Kagera kwa kushirikiana na **Ofisi ya Taifa ya Mashitaka** tutamfikisha katika Mahakama ya Hakimu Mkazi **Bw. SHAMI YAHAYA MAGETHA**

ambaye ni mtumishi wa TANESCO (Fundi) Wilaya ya Karagwe kwa makosa ya matumizi mabaya ya ofisi na kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu.

Ndugu wanahabari,

Katika uchunguzi uliofanyika imethibitika kuwa kati ya mwezi machi na Aprili mwaka 2019 Bw **SHAMI YAHAYA MAGETHA** akiwa mtumishi wa TANESCO (Fundi) wilaya ya Karagwe na akiwa na nia ya kujipatia fedha alipeleka Nguzo ya Umeme - kwa lengo la kumuunganishia huduma ya Umeme mtu mmoja ambaye jina lake limehifadhiwa na kisha kujipatia kiasi cha shilingi laki tano (Shs 500,000/=) katika kijiji cha Luzinga Kata ya Bugeme kinyume cha taratibu za TANESCO na huku akijua kuwa eneo hilo lilikuwa katika Mpango wa kupelekewa Umeme chini ya mradi wa REA.

Ndugu wanahabari,

Uchunguzi wetu umeweza kuthibitisha pia kuwa wakati Bw. **SHAMI YAHAYA MAGETHA** akipeleka Nguzo hiyo hakuwa amepewa kibali cha kufanya hivyo kutoka kwa Mkandarasi wa mradi wa REA. Aidha meneja wa TANESCO wilaya ya Karagwe hakuwa anaifahamu kazi hiyo na hakutoa kibali cha kufanyika kwa kazi hiyo.

Kutokana na Nguzo hiyo kupelekwa na kujengwa kinyume cha taratibu na fedha alizotoa mteja kutowasilishwa TANESCO, uongozi wa TANESCO wilaya ya Karagwe mara baada ya kubaini uwepo wa Nguzo hiyo iliyojengwa kinyume cha taratibu za TANESCO uliamua kuing'oa .

Ndugu wanahabari,

Kutokana na sababu hiyo, mtuhumiwa **SHAMI YAHAYA MAGETHA** atafikishwa mahakamani kwa makosa matumizi mabaya ya ofisi chini ya kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sheria namba 11/2007 na kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu chini ya kifungu cha 302

cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura namba 16 (**kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002**)

Ndugu wandishi wa habari,

Pia naomba nitoe wito kwa wana Kagera wote kwa ujumla kuwa ni vyema wakati wote tunapotekeleza majukumu yetu kuhakikiasha tunazingatia Sheria , Kanuni na Taratibu. Aidha ikumbukwe kuwa kwa mujibu wa maandishi matakatifu ya BIBILIA na QU'RAN Rushwa ni dhambi, hivyo tusikubali kushiriki katika dhambi kwani kwa kufanya hivyo tunaweza kupata laana kutoka kwa Mwenyezi Mungu (SW) kama ilivvofafanuliwa katika Sunan Abu Dawood katika hadithi namba 3573(Rejea QU'RAN TUKUFU)

Hitimisho

Rushwa ni adui wa haki na inaweza kuathiri mgawanyo wa rasilimali katika jamii na kusababisha wananchi kukata tamaa. Hivyo ni wajibu wa kila Mtanzania kuchukua hatua kila anapoona kuna dalili ya vitendo vya rushwa kufanyika na ni vyema kila mmoja wetu kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi zilizowekwa kwa maslahi mapana ya Taifa. Hivyo nitoe wito kwa Wananchi wote kuchukua hatua mahususi pale wanapoona kuna dalali au ukuikwaji wa sheria zetu za nchi au kuna viashiria vya uwepo wa vitendo vya rushwa.

Imetolewa na:

Signed

JOHN K.E JOSEPH

MKUU WA TAKUKURU (M)

